**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE UZINDUZI WA JENGO LA SARATANI BUGANDO

**13 SEPTEMBA, 2022**

- **Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb), Naibu Waziri wa Afya;**
- **Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote mliopo hapa;**
- **Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;**
- **Mhashamu Renatus Nkwande, Askofu Mkuu - Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza na Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando;**
- **Wahashamu Maaskofu wote mliopo;**
- **Waheshimiwa sana Mapadre, Mashemasi na Watawa wote;**
- **Mheshimiwa Marco Lombardi, Balozi wa Italia nchini Tanzania;**
- **Mheshimiwa Binaya Srikanta Pradhan Balozi wa India nchini Tanzania;**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa Mikoa na Wakuu wa Wilaya mliopo;**
- **Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza;**
- **Viongozi wote wa Chama na Serikali mliopo;**
- **Ndugu Dr. Fabian Massaga, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando;**
- **Watumishi wote wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando;**
- **Viongozi wote wa Madhehebu mengine ya Dini;**
- **Wadau wote wa Maendeleo mliopo;**
- **Ndugu Wananchi wa Mwanza;**
- **Ndugu Wanahabari;**
- **Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.**

**TUMSIFU YESU KRISTO!**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, neema na afya njema na pia kutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo kushiriki tukio

hili muhimu la uzinduzi wa Jengo hili la Saratani hapa Bugando Mwanza. Aidha, nawashukuru sana wana Mwanza na uongozi mzima wa Hospitali ya Bugando kwa mapokezi mazuri. **Asanteni sana!** Nawashukuru wote mliofika hapa kwa ajili ya kuungana nasi katika tukio hili muhimu.

Nichukue fursa hii pia kwa niaba ya Serikali kulipongeza na kulishukuru Kanisa Katoliki na taasisi zetu zote za dini hapa nchini kwa kuunga mkono juhudi za Serikali na kwa kutoa mchango mkubwa sana katika ustawi wa Taifa letu kiroho, kiuchumi na kijamii. Mmeweza kufikisha huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwemo yale ambayo Serikali bado haijaweza kufikisha huduma hususan vijijini na maeneo wanakoishi watu wa hali ya chini mijini. Wananchi wameweza kupata huduma bora za afya na elimu hasa kwa watu wa kawaida, yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Mwenyezi Mungu azipokee kazi zenu njema.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Takwimu zinaonesha kuwa ugonjwa wa saratani bado ni miongoni mwa magonjwa yanayoongoza duniani kwa kusababisha vifo kwa watu wengi. Hapa nchini, ugonjwa huu wa saratani bado unaendelea kuongezeka ambapo kwa sasa takwimu zinaonesha kila mwaka takribani watu 42,000 hupata ugonjwa huu wa saratani. Hii ni idadi kubwa na ndio maana Serikali imeamua kwa dhati kuongeza mapambano dhidi ya ugonjwa huu na magonjwa mengine yasioambukiza.

Serikali yetu imewekeza katika kutekeleza afua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza. Miongoni mwa mikakati iliyopo ni pamoja na kupunguza vihatarishi vya magonjwa haya kwa kuelimisha jamii kuchukua hatua stahiki za kuboresha mtindo wa maisha kwa kuzingatia ulaji unaofaa, kupunguza matumizi ya pombe, kuacha matumizi ya tumbaku, kufanya mazoezi na kuepuka tabia bwete. Mtindo wa maisha usiofaa ni miongoni mwa vihatarishi vikubwa vya magonjwa mengi yasiyoambukiza ikiwemo saratani.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Zoezi la uchunguzi wa mapema wa saratani ni miongoni mwa mbinu muhimu katika kukabiliana na tatizo hili. Saratani ikitambuliwa mapema inaweza kutibika kabisa. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwenye sekta ya afya, imekuwa ikifanya uchunguzi wa saratani katika makundi hatarishi. Mwaka 2021 takribani wanawake 365,164 walifanyiwa uchunguzi. Miongoni mwa hao jumla ya wanawake 8,762 walibainika kuwa na dalili za awali za saratani ya

shingo ya kizazi. Aidha katika kipindi cha mwaka 2021/22 Serikali iliweka malengo ya kuwafikia wasichana 689,280 wenye umri wa miaka 14 kwa ajili ya chanjo dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi ambayo inaongoza kuathiri wanawake wengi zaidi. Katika zoezi hilo jumla ya wasichana 535,298 sawa na asilimia 78 ya wasichana waliokusudiwa walipata Dozi ya Kwanza ya Chanjo hiyo (HPV1). Aidha, jumla ya wasichana 420,015 sawa na asilimia 61 ya wasichana waliokusudiwa walirudi kwa ajili ya kukamilisha dozi ya pili. Hii inamaana kuwa bado wasichana wengine hawakukamilisha dozi hiyo. Hivyo kupitia hadhara hii, ninawasihi sana vijana wetu kupata chanjo hizi kwa ukamilifu kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya. Nawaomba sana wazazi tushirikiane na Serikali kuhakikisha vijana wetu wanapata chanjo hii muhimu ili waweze kujikinga na gonjwa hili hatari la saratani.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;***

Serikali inawekeza kwenye miundombinu ili kuhakikisha huduma za matibabu ya saratani zinasogezwa karibu na wananchi. Awali wagonjwa wote wa saratani walikuwa wakitibiwa kwenye Taasisi ya Ocean Road pekee iliyopo Dar es Salaam. Lakini hadi kufikia mwaka 2020, kuna jumla ya Hospitali kumi na tatu zinazotoa huduma za matibabu ya ugonjwa huu ambapo kati ya hizo, Hospitali sita ni za umma, ikiwemo Hospitali yetu hii ya Bugando. Aidha, itakumbukwa pia, kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Serikali ya India na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, Serikali iliweka mashine za tiba ya mionzi zilizoanza kutumika mwaka 2017. Kama wataalamu wetu walivyosema, kuanzishwa kwa huduma ya tiba mionzi hapa Bugando kulisababisha ongezeko kubwa la wagonjwa waliokuja kupata tiba hii na hivyo kufanya miondombinu iliyokuwepo kutotosheleza kulaza wagonjwa. Hata hivyo, pamoja na changamoto hiyo, uwepo wa Mashine hizi umeleta unafuu mkubwa kwa wananchi wengi wa Mikoa ya kanda ya ziwa na ile ya magharibi mwa nchi yetu ambapo hapo awali walilazimika kusafiri hadi Dar es Salaam ili kufuata huduma hizi za matibabu ya Saratani.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Katika ujenzi wa Jengo hili linalozinduliwa leo, ambalo limegharimu kiasi cha shilingi bilioni 5.5, Serikali imechangia jumla ya Shilingi Bilioni 2.9 ambapo tayari Bilioni 1.9 imeshapokelewa na kiasi kingine cha Bilioni 1 kimetengwa kwenye bajeti ya mwaka huu 2022/23. Aidha, natoa pia pongezi kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali, Mkurugenzi na Menejimenti yake kwa kuridhia matumizi ya Shilingi

Bilioni 3 kutoka vyanzo vyenu vya ndani kwa ajili ya mradi huu. Hali kadhalika, kipekee kabisa natoa pia pongezi kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Bugando kwa kuamua kuwa sehemu ya maendeleo haya kwa kuchangia fedha zenu binafsi, jumla ya Shilingi milioni 250. **Hongereni sana!** Tendo hili ni la kizalendo na utu na linaonesha ni kwa namna gani mnajali afya za watanzania. Mwenyezi Mungu awabariki kwa wema wenu huu na upendo mliouonesha kwa watanzania. Vilevile, naomba niwashukuru pia wakazi wa kanda ya ziwa na wadau wote ambao wamechangia zaidi ya Shilingi milioni 450 kufanikisha ujenzi huu. Naomba niwahakikishie, fedha yenu itatumika kama ilivyokusudiwa na kwenye hili nakuagiza Waziri wa Afya usimamie kikamilifu.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Ujenzi wa jengo hili litakalokuwa na vitanda 120 vya wagonjwa ni hatua kubwa kuelekea kutoa huduma bora za matibabu ya Saratani katika Kanda ya Ziwa. Hivyo natoa wito kwenu wana Bugando kulitunza jengo hili na hospitali yetu yote ili iweze kusaidia wananchi kwa miaka mingi ijayo. Nafahamu pamoja na kukamilika kwa jengo, kuna baadhi ya huduma hazitaweza kutolewa kwa sasa. Kama alivyoelezea Mwenyekiti wa Bodi, bado tutahitaji kuboresha mitambo ya matibabu ya radiolojia na ununuzi wa vifaa vingine ambavyo vinaweza kugharimu zaidi ya Shilingi Bilioni 15. Serikali imeyasikia maombi yenu na ninakuelekeza Mheshimiwa Waziri wa Afya kufanyia kazi maombi haya. Naomba nirudie tena kuwashukuru sana Bodi ya wadhamini na uongozi wote wa Hospitali ya Bugando kwa kuwa na mipango mizuri ya maendeleo inayochangia kuongezeka kwa wigo wa utoaji wa huduma za matibabu ya Saratani katika Kanda ya Ziwa.

Mwisho, napenda kutumia fursa hii kulishukuru Kanisa Katoliki na Madhehebu mengine kwa kuendelea kushirikiana na Serikali kusogeza huduma za jamii ikiwemo afya karibu na wananchi. Ni matuamini yangu kuwa, mahusiano haya mazuri kati ya Serikali na Taasisi za Dini yataendelea na Serikali ipo tayari kushirikiana na wadau wengine ili kuendelea kuboresha huduma za afya hapa nchini.

**Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa Jengo la Saratani hapa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando limefunguliwa rasmi.**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**.